

Ofisi za Idara:

1700 - 155 Carlton St.
Winnipeg MB R3C 3H8
Nambari ya simu.
204-945-2476
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-782-8403
Nambari ya kutuma Faxi:
204-945-6273
Anwani ya mtandao:
rtb@gov.mb.ca

143-340 9th Street
Brandon MB R7A 6C2
Nambari ya simu.
204-726-6230
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-656-8481
Nambari ya kutuma Faxi:
204-726-6589
Anwani ya mtandao:
rtbbrandon@gov.mb.ca

113-59 Elizabeth Dr.
Thompson MB R8N 1X4
Nambari ya simu.
204-677-6496
Nambari ya simu isiyo na
malipo: 1-800-229-0639
Nambari ya kutuma Faxi:
204-677-6415
Anwani ya mtandao:
rtbthompson@gov.mb.ca

The Residential Tenancies Branch Idara ya Kupangisha Makaazi

MAMBO MAALUM

Majukumu ya Wapangishaji na Wapangaji

Mpangishaji lazima:

- **Ahakikishe kwamba nyumba iko tayari kwa mpangaji kwa tarehe iliyokubaliwa;**
- **Apeane risiti ya kodi ikiwa kodi inalipwa kwa pesa taslimu. (Pesa ambayo imepangiwa kuondatelewa kwenye benki awali inachukuliwa kama pesa taslimu); risiti lazima ionyeshe kiasi cha pesa iliyopokelewa, tarehe pesa ilipopokelewa, na anwani ya chumba na mjengo;**
- **Ahakikishe kwamba chumba kimewekwa kwa hali nzuri, kuzingatia mda wa upangishaji;**
- **Atengeneze chumba panapo haja na ahakikishe kuwa chumba kiko kwa hali nzuri;**
- **Ahakikishe kwamba mahitaji ya lazima yapo, kwa mfano moto, sitima, maji ya moto na baridi;**
- **Asiingilie kwa vyovyote na mahitaji haya ya lazima;**
- **Aruhusu mpangaji au jamaa ya mpangaji kutumia chumba au makaazi kwa kila hali ya kawaida;**
- **Achunguze kwa haraka iwezekanavyo malalamishi kuhusu kusumbuliwa au usalama na ajaribu kutatua shida;**
- **Apeane na adumishe usalama kwa kupeana milango na kufuli.**

(pindua ukurasa)

Mpangaji lazima:

- **Alipe kodi kwa wakati;**
- **Adumishe usafi wa chumba na makaazi;**
- **Apokee ruhusa kwa maandishi kutoka kwa mpangishaji kabla ya kupaka rangi au kubadilisha hali ya chumba;**
- **Ajitahadharishe na kuharibu chumba, na ikiwa ataharibu chochote, atengeneze madhara vizuri katika mda unaofaa;**
- **Asisumbue wengine katika jengo au majengo jirani;**
- **Asihatarishe maisha ya wengine walioko kwenye jingo;**
- **Ahakikishe kwamba watu anaoruhusu kuja chumbani hawataharibu, sumbuua au kuhtatarisha usalama wa wengine;**
- **Atii sheria na desturi za mpangishaji;**
- **Aeleze mpangishaji kuhusu chochote kinachohitajika kutengenezwa.**

Kwa maelezo zaidi

Karatasi hii ya mambo muhimu inapeana maelezo machache tu. Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, wasiliana na:

Idara ya Kupangisha Makaazi